JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Barabara ya Kilimatinde Cheyo,
S.L.P. 1020,
45112
TABORA,
Barua Pepe: rbctabora@pccb.go.tz.
TANZANIA.

TAARIFA YA UTENDAJI KAZI JANUARI HADI MACHI 2023

TABORA – Mei 10, 2023

TAKUKURU Mkoa wa Tabora kwa kipindi cha **Januari 2023 hadi Machi 2023** imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na 11/2007 kama yalivyoainishwa katika kifungu cha 7. Utekelezaji wa majukumu hayo umefanyika kwa kuendelea kufanyia kazi malengo tuliyojiwekea kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa kazi za Uchunguzi, Elimu Kwa Umma na Uzuiaji Rushwa.

1. UZUIAJI RUSHWA

Katika kipindi cha Januari - Machi 2023 TAKUKURU Mkoa wa Tabora imefanya **chambuzi za mifumo 11, Warsha 4**, na kufuatilia utekelezaji wa **miradi 18** yenye tahamani ya **shilingi 662,704,346,141.01.** Katika ufuatiliaji huo, Miradi miwili yenye thamani ya sh **569,519,950** ilikutwa na mapungufu na hatua mablimbali zilichukuliwa kama ifuatavyo:-

1.1 UFUATILIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

S/N	MIRADI ILIYOFUATILIWA NA THAMANI YAKE	YALIYOBAINIKA	HATUA ZILIZOCHUKULIWA
1	Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Ujenzi wa Madarasa matatu na Ofisi moja katika Shule ya Sekondari Isevya. Mradi huu una thamani ya	Wakati wa Utekelezaji kulikuwa na mfumuko wa bei uliosababisha gharama za ujenzi kuongezeka tofauti na bajeti iliyopangwa.	Elimu imetolewa kwa kamati na kuwashauri wafuate taratibu za manunuzi na kujipanga mapema ili kuepukana na changamoto kama hii.

	Sh. 60,000,000/=		
2	Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi inayotekelezwa na wanufaika wa mikopo ya 10% inayotolewa na Halmashauri yenye thamani ya **Shs 509,519,950/=**	Vikundi kukiuka masharti ya mkopo kwa kugawana fedha za mkopo hivyo kutokuwepo kwa miradi ya pamoja.	Elimu imetolewa kwa wanakikundi kuhakikisha wanafuata masharti ya mikopo hiyo. Hata hivyo serikali imesitisha utoaji wa mikopo hii hadi utaratibu mwingine utakapoandaliwa

Ifuatayo ni taarifa ya uchambuzi wa mifumo, yaliyobainika na hatua zilizochukuliwa:-

1.2 UCHAMBUZI WA MIFUMO

S/N	MFUMO ULIOCHAMBULIWA	YALIYOBAINIKA	HATUA ZILIZOCHUKULIWA
1	Mianya ya rushwa katika mfumo wa ukusanyaji wa Mazao ya Misitu.	Ukiukwaji wa Sheria na Taratibu kwenye uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu Ufujaji wa fedha kwenye ukusanyaji wa mapato yanayotokana na mazao ya misitu	Kuandaa kikao cha wadau kwa ajili ya kuweka maazimio ya kurekebisha kasoro zilizobainika Mpango Mkakati wa kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa katika uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu umeandaliwa na unatekelezwa na ofisi ya TAKUKURU (M).
2	Upimaji na Urasimishaji wa Ardhi - Manispaa ya Tabora - Januari - Machi 2023	Utofautianaji wa gharama za upimaji na urasimishaji katika eneo moja	TAKUKURU kuitisha kikao cha wadau ili kuweka maazimio ya kurekebisha kasoro zilizobainika

2. ELIMU KWA UMMA

Jamii imeendelea kupatiwa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa katika nyanja mbalimbali ili iendelee kuonesha ushirikiano katika mapambano dhidi ya rushwa. Elimu hiyo imelenga kuwajengea uwezo wananchi sio tu katika kutoa taarifa za vitendo vya rushwa bali pia kushiriki kikamilifu katika kuibua kero mbalimbali zilizopo katika jamii na kutoa mapendekezo yatakayotatua kero hizo zinazoweza kusababisha vitendo vya rushwa kujitokeza. Mchanagnauo wa kazi hizo ni ufuatao: -

Na.	KAZI
1	Semina 17 zilifanyika
2	Mikutano ya hadhara na mijadala ya wazi 37
3	Makala 07 ziliandikwa
4	Vipindi vya redio 03
5	Kuimarisha klabu 103
6	Maonesho 05

2.1 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA TAKUKURU RAFIKI:

IDADI YA KATA ZILIZOFIKIWA	IDADI YA KERO ZILIZOTOLEWA	IDADI YA KERO ZILIZOTATULIWA	MIFANO YA KERO ZILIZOTATULIWA NA SEKTA YAKE KTK MABANO	MAFANIKIO YA TR KATIKA MKOA WAKO KWA KIFUPI
14	176	46	Umeme haujasambaa mitaani katika majumba hasa Lugubu Mashariki na Lugubu Magharibi [NISHATI] –	Nguzo za umeme zimesambazwa na kusimikwa katika mitaa ya Lugubu Mashariki na Maghariki na hivyo kuitatua kero hii.
			Kuzagaa kwa punda, ng'ombe, mbuzi na mifugo mingine ambayo imekuwa ikifanya uharibifu mashambani (Kilimo)	Kuzagaa kwa mifugo kumepungua na wanacnhi wamejenga mazizi ya kutunza mifugo yao.

			Wananchi kukosa elimu juu ya vigezo na masharti ya kupata mikopo ya Halmashauri ya 10% inayotolewa kwa wanawake, walemavu na vijana.	Maafisa maendeleo ya jamii kutoa elimu kwa vikundi vya wajasiriamali kuhusiana na vigezo vya kupata mikopo hiyo. Elimu hiyo ilitolewa wakati wa kusikiliza kero lakini pia wameahidi kupita kwenye kata kutoa elimu.

2.2 USHIRIKIANO NA WADAU

S/N	SHUGHULI	KAULI MBIU	WADAU WALIOSHIRIKISHWA	KAZI ILIYOFANYIKA
1	Uelimishaji wa pamoja katika Maadhimisho ya Wiki ya Sheria mwaka 2023	"Umuhimu wa Utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi katika kukuza uchumi endelevu wajibu wa Mahakama na wadau"	TAKUKURU pamoja na wadau wengine wa sheria na Idara ya Mahakama. Wadau wengine walikuwa ni: Mwanasheria Mkuu Wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu Wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Chama cha Mawakili wa Kujitegemea Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, watoa Huduma za Msaada wa Kisheria, Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza.	Kushiriki maandamano ya kufungua Wiki ya Sheria, kutoa elimu kupitia maonesho kwa wananchi waliotembelea banda la TAKUKURU, kutoa elimu kwenye Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo na Taasisi za Dini.
2	MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI	Ubunifu na Mabadiliko ya Teknolojia, chachu katika kuleta usawa wa Kijinsia"	Chama Cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU)	Kushiriki Kongamano la Siku ya wanawake duniani, Kutoa misaada ya kibinadamu kwenye Gereza la Wanawake (Gereza la ZUBERI.) Kushiriki Maonesho ya Kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake duniani.

3. UCHUNGUZI NA MASHTAKA

Katika kipindi husika malalamiko yaliyopokelewa ofisini ni **97,** kati ya hayo **65** yalihusu rushwa na malalamiko **32** hayakuhusu rushwa. Kwa malalamiko yaliyohusu rushwa uchunguzi unaendelea kuthibitisha tuhuma na kwa yale ambayo hayakuhusu rushwa, malalamiko **27** wahusika wameshauriwa na malalamiko **5** yamehamishiwa idara nyingine.

Sekta zilizolalamikiwa na idadi yake ni Tamisemi 59, Mahakama 8, Polisi 4, Ardhi 6, Ujenzi 3, Manunuzi 2, Afya 3, Mazingira 1, Taasis za Fedha 3 (FAIDIKA, ACCESS BANK, MABOTO CREDIT SERVICES), Nyinginezo 8.

Majalada yaliyokamilika ni 13, Majalada yaliyopata kibali cha DPP ni 1, Kesi mpya zilizofunguliwa mahakamani 8 na Kesi zilizotolewa maamuzi na Jamhuri kushinda 3.

MIKAKATI YA APRILI - JUNI 2023

TAKUKURU Mkoa wa Tabora itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na kushirikiana na wadau mbalimbali katika mapambano dhidi ya Rushwa. Tutajikita katika Kuzuia vitendo vya rushwa visitokee kwa kutoa elimu ya kutosha kwa taasisi mbalimbali na jamii kwa ujumla ili kuhakikisha wananchi sio tu wanaifahamu na kuichukia Rushwa bali kuongeza mwamko wao katika kutoa Taarifa za vitendo vya Rushwa vinavyojitokeza katika mazingira yao.

WITO KWA WAKAZI WA MKOA WA TABORA

Ninatoa wito kwa wakazi wa Mkoa wa Tabora na watanzania wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU hasa katika Kuzuia vitendo vya rushwa visitokee na kusubiri mpaka ubadhirifu kufanyika na Serikali kupoteza fedha ndipo watoe taarifa. Endeleeni kuelimishana kupitia elimu inayotolewa na TAKUKURU na kushiriki kikamilifu kwenye utekelezaji wa Programu ya TAKUKURU Rafiki kwa kuhakikisha mnafika kwenye vikao vinayoandaliwa ili muweze kutoa kero zenu na kushirki kwenye utatuzi wa kero hizo.

"KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU"

Imetolewa Na:

MUSA CHAULO
MKUU WA TAKUKURU Mkoa wa TABORA
0738 - 150218